



HALMASHAURI YA
MANISPAA YA
SONGEA

TOLEO MAALUM LA MRADI WA ULGSP

MANISPAA YA SONGEA

NOVEMBA 2019

**Manispaa ya Songea inavyonufaika na miradi ya
ULGSP**

YALIYOMO

MACHINJIO YA KISASA SONGEA	2
KITUO KIKUU CHA MABASI SONGEA	3
BARABARA ZA LAMI NZITO KM 10.3	4
BUSTANI MANISPAA YA SONGEA	5
STENDI YA MFARANYAKI	6
WATUMISHI KUJENGEWA UWEZO	7



Rais Dkt John Magufuli akikata utepe wa jiwe la Msingi katika ujenzi wa Kituo kikuu cha mabasi Mkoa wa Ruvuma katika Kata ya Tanga Manispaa ya Songea

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea ni Miongoni mwa Halmashauri 18 nchini zinayotekeleza Mradi wa uendelezaji Miji na Manispaa unaotekezwa kwa fedha za Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (ULGSP). Lengo la ULGSP ni kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, machinjio, vituo vya mabasi, maeneo ya mapumziko, kuongeza mapato na kujenga uwezo kwa watumishi ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma bora kwa

Miradi hii ikikamilika itasaidia kuongeza mapato ya Halmashauri, kutoa ajira kwa wananchi na kuongeza barabara za lami toka kilometa 16 mwaka 2021/2013 hadi kufikia kilometa 26.3 mwaka 2019/2020.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea imefanikiwa kufuzu vigezo kwa kupata fedha za ULGSP kwa miaka sita kiasi cha shilingi bilioni 32.

Manispaa ya Songea inatekeleza miradi mitano kupitia ULSP

Miradi hiyo ni ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Kata ya Tanga ambayo inatarajiwa kuongoza kwa ubora Tanzania, mradi wa ujenzi wa barabara ya lami nzito zenye urefu wa kilometa 10.3, ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi katika Mkoa wa Ruvuma, stendi ndogo ya Mfaranyaki na bustani ya Manispaa

Mradi wa machinjio ya kisasa

MACHINJIO YA KISASA ILIYOPO KATA YA TANGA MJINI SONGEA



Hata hivyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea Tina Sekambo amesema kuwa kazi iliyobaki ni uwekezaji wa vifaa katika machinjio hiyo ili iweze kuanza kazi Mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka huu.

Gharama ya mradi huu ni jumla ya **Tshs. 3, 216, 237,382.4** Mpaka sasa Mkandarasi ameshalipwa kiasi cha **Tshs. 1, 924, 419,648.4** Machinjio hii itakapokamilika itaongeza idadi ya ng'ombe wanaochinjwa katika Manispaa kutoka Ng'ombe 32 kwa siku mpaka Ng'ombe 200 kwa siku na kuongeza ubora wa bidhaa nyama. Kukamilika kwa machinjio hii kutafungua fursa mpya za ajira kwa wananchi wa Manispaa ya Songea na wataanzania kwa ujumla

MRADI wa machinjio ya kisasa katika Kata ya Tanga Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Julai, 2017, hadi sasa ujenzi wa machinjio ya kisasa umekamilika kwa asilimia 100.

Mradi wa kituo kikuu cha mabasi cha Mkoa wa Ruvuma

MUONEKANO WA STENDI YA MABASI YA KISASA YA MKOA WA RUVUMA AMBAYO INAJENGWA KATIKA KATA YA TANGA MANISPAA YA SONGEA



MRADI UMEFADHILIWA NA BENKI YA DUNIA KWA SHILINGI BILIONI SITA UJENZI UMEFIKIA ZAIDI YA ASILIMIA 90, STENDI ITAFUNGULIWA MWEZI DESEMBA 2019



UJENZI wa kituo kikuu cha mabasi unafanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekari **15** lilipo katika Kata ya Tanga kilomita **12** toka katikati ya Manispaa ya Songea kwa gharama ya zaidi ya bilioni sita. Ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi Songea, ulianza tarehe 25/03/2018 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30/09/2019. Ujenzi unafanywa na Mkandarasi CHINA SICHUAN INTERNATIONAL CORPORATION (SIETCO).

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo anasema Mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nzito zinazolingia, kutoka na kuzunguka kituo cha mabasi zenye urefu wa kilomita mbili. Upana wa barabara zinazolingia na kutoka ni mita saba na barabara zinazozunguka kituo cha mabasi ni mita 12.

Kwa mujibu wa Sekambo, Mradi huu pia unahusisha, Ujenzi wa mifereji ya barabara na Ujenzi wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba **17,100** la kugesha mabasi lenye uwezo wa kugesha mabasi **92** kwa wakati mmoja. Vilevile kutakuwa na vibanda vya abiria kusubiria mabasi (shadee) **48**. Sekambo anasema Stendi ya mabasi ya Songea pia inahusisha Ujenzi wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba **1800** la kugesha Taxi lenye uwezo wa kugesha Taksi **60** kwa wakati mmoja, Ujenzi wa Uzio mita **900**. Ujenzi wa maduka **30** na Ujenzi wa ofisi za kukatia tiketi **20**.

“Maeneo mengine yanayohusika na mradi huu ni Ujenzi jengo la Utawala, Ujenzi wa vyoo,

Ujenzi wa barabara za lami nzito Manispaa ya Songea

UJENZI WA BARABARA ZA LAMI NZITO KM 10.3 KATIKA MANISPAA YA SONGEA WAFIKIA ASILIMIA ZAIDI YA 95



Mkandarasi alishindwa kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba, hivyo Halmashauri ilisitisha mkataba wa Matengenezo ya Barabara.

kazi ya Ujenzi wa barabara km 10.3 kwa kiwango cha lami ilitangazwa tena mwezi Oktoba 2017 na kupatikana kwa mkandarasi **M/S CHINA SICHUAN INTERNATIONAL CO-OPERATION CO. LTD.**

Mradi huu umeanza kutekelezwa mwezi Machi, 2018 na unategemewa kukamilika mwezi Septemba, 2019. Mpaka sasa

Mkandarasi ameshalipwa kiasi cha **Tshs. 6,038,006,039.65** ikiwa ni malipo ya awali pamoja na kazi ambazo ameshafanya mpaka sasa hivi. Mradi umefikia asilimia 45 ya utekelezaji. Mradi huu baada ya kukamilika utagharimu kiasi cha **Tshs. 13,104,078,000.20** ikiwa ni gharama alizolipwa mkandarasai

Ujenzi wa barabara kiwango cha lami km 8.6 katika barabara za katikati ya Mji ulianza kutekelezwa tarehe 01 Juni, 2015 na ulitarajia kukamilika tarehe 30 Juni, 2017 chini ya Mkandarasi M/s Lukolo Co Ltd.

Gharama ya mradi ilikuwa ni **Tshs. 14,320,586,464.39** (pamoja na VAT). Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2017 Mkandarasi alilipwa kiasi cha **Tshs. 2,204,887,742.00**

wa awali pamoja na mkataba mpya unaoendelea. Kukamilika kwa mradi huu utarahisisha mawasiliano, kuongeza fursa za kiuchumi na usafirishaji wa bidhaa na mazao.

Mradi wa Bustani ya Manispaa ya Songea

BUSTANI YA MANISPAA YA SONGEA ILIYOBADILISHA MUONEKANA WA MJI WA SONGEA, INAVUTIA WENGI



MUONEKANO WA BUSTANI YA MANISPAA YA SONGEA



HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imetumia jumla ya sh.milioni 400 kwa ajili ya uboreshaji wa Bustani ya Manispaa ya Songea.

Mradi huo uliofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya Mpango wa Kuzijengea uwezo serikali za mitaa(ULGSP) umegharimu sh.milioni 399.95 na umekamilika kwa asilimia 100.

Mradi huo uliopo mkabala ya Ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Songea una eneo la mgahawa,choo cha kulipia,uzio na maeneo ya kupaki magari(parking bay).

Bustani hiyo ya aina yake katika mji wa Songea ina eneo la kupumzikia(resting huts) .

Maeneo mengine katika bustani hiyo ni uzio kuzunguka bustani yote. bustani pia imewekwa u dongo na kupandwa nyasi na miti na ujenzi wa mnara.

Manispaa ya Songea ni moja ya Halmashauri za miji na Manispaa 18 za Tanzania Bara ambazo zipo katika mpango wa ULGSP lengo likiwa ni kuendeleza miundombinu yake.

Halmashauri nyingine ambazo zinanufaika kupitia mradi wa ULGSP ni Sumbawanga, Singida, Tabora, Shinyanga, Musoma,Moshi,Lindi, Morogoro, Iringa, Babati, Msasi, Kibaha, Njombe, Mpanda,Korogwe na Geita.



Mradi wa ULGSP ulivyowajengea uwezo watumishi wa Manispaa

MANISPAA YA SONGEA YAWAJENGEA UWEZO WALIMU 50 WANAOFUNDISHA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM



MAFUNZO YAMEFUNGULIWA NA POLOLET MGEMA MKUU WA WILAYA YA SONGEA NA KUFUNGWA NA TINA SEKAMBO MKURUGENZI WA MANISPAA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea kupitia fedha za kuwajengea uwezo watumishi (ULGSP) imetoa mafunzo kwa walimu 50 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi na sekondari.

Akizungumza kabla ya kufungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Songea Pololet Mgema amesema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa walimu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali wakiwemo wanafunzi wasioona, wasiosikia, wenye ulemavu wa akili na wenye ulemavu zaidi ya mmoja ili walimu waweze kutoa elimu kwa ufanisi.

Amesema serikali kwa kutambua uwepo wa wanafunzi wenye mahitaji maalum, imeweka mazingira ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata elimu sawa, ndiyo maana serikali imeanzishwa vyo vya elimu maalum.

Kwa mujibu wa Mgema, mafunzo hayo yatawawezesha walimu ambao hawakupata mafunzo maalum, kuweza kutambua mambo muhimu kama lugha za alama na maandishi ya nukta nundu ili waweze kusaidia kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Kwa upande wake Afisa Elimu maalum katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Rehema Nyagawa amesema katika Manispaa hiyo kuna jumla ya wanafunzi 405 wenye mahitaji maalum kati yao wavulana 243 na wasichana 162.

Nyagawa amesema Manispaa ya Songea ina jumla ya walimu 52 tu waliosomea kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum na kwamba kuna walimu 12 ambao wanafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum bila kusomea elimu maalum.

“Manispaa ya Songea ina upungufu wa walimu wenye mahitaji maalum 13, jumla ya walimu 65 wanahitajika, ”, alisema Nyagawa.

Watumishi wa Manispaa ya Songea walivyonufaika na ULGSP



MKUU wa Idara ya Utumishi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Lewis Mnyambwa anasema kwa kiwango kikubwa watumishi katika Manispaa hiyo wakiwemo madiwani wamefaidika kwa mafunzo na vifaa kupitia mradi wa ULGSP.

Amesema madiwani wamepata mafunzo katika maeneo ya usimamizi wa mikataba, miradi na mafunzo ya usimamizi wa ukusanyaji mapato katika Halmashauri.

Amesema kwa kutumia kifungu cha fedha za kujenga uwezo, madiwani pia walipelekwa kwenye ziara za mafunzo Morogoro na Dodoma.

Hata hivyo Mnyambwa amesema katika eneo la mafunzo kwa watumishi, mradi wa ULGSP umenufaisha katika kiwango kikubwa na kwamba karibu kila Idara imeguswa katika maeneo ya kuwajengea uwezo.

“Tulikuwa na upungufu mkubwa wa vitendeakazi kwa watumishi hasa kompyuta na samani mbalimbali, kupitia mradi huu tumeweza kununua kompyuta katika Idara zote na samani zake”, alisema Mnyambwa.

Ameongeza kuwa kupitia ULGSP, Halmashauri imeweza kuboresha vifaa vya kisasa kwenye ukumbi na kununua vifaa vya ofisi katika baadhi ya ofisi za kata na baadhi ya ofisi za mitaa katika Manispaa ya Songea.

Kwa upande wake Msimamizi na mfuatiliaji wa miradi ya ULGSP katika Manispaa ya Songea Upendo Bonamali akizungumzia kwa ujumla namna miradi hiyo ilivyowanufaisha watumishi na madiwani amesema katika kipindi cha miaka mitano kupitia ULGSP mafunzo yametolewa kwa madiwani 30, wenyeviti wa mitaa 95 na viongozi wengine ngazi ya mitaa zaidi ya 300 wamepata mafunzo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Bonamali katika kipindi hicho Manispaa ya Songea imeweza kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya watumishi zikiwemo kompyuta mpakato 46, kompyuta za mezani 28, printa 26 na mashine za kielektoniki za kukusanyia mapato (POS) 110.

Vifaa vingine anavitaja kuwa ni kabinetu 107, viti 365, meza 31 na vifaa vingine katika Idara mbalimbali na kwamba kupitia mradi wa ULGSP umefanyika ukarabati wa baadhi ya ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Songea na ujenzi wa masijara kuu ya Manispaa ya Songea.



**HALMASHAURI YA
MANISPAA YA SONGEA**

MAWASILIANO

S.L.P 14 SONGEA

Simu ya Mezani: 025 260297

Nukushi: 025 2602474

Simu ya mkononi :0784765917

Baruapepe:info@songeamc.go.tz

Tovuti:www.songeamc.go.tz

BODI YA UHARIRI

1.TINA SEKAMBO

MKURUGENZI WA MANISPAA
SONGEA

2.ALBANO MIDELO

AFISA HABARI MANISPAA
YA SONGEA

3.UPENDO BONAMALI

AFISA TAKWIMU MANISPAA



Stendi ya Mfaranyaki yaongeza mapato kwa asilimia 300



Halmashauri ya Manispaa ya Songea imeanza kunufaika na mradi wa kituo kidogo cha mabasi cha Mfaranyaki ambacho kimekarabatiwa na Benki ya dunia kwa gharama ya shilingi milioni 550.Ukusanyaji wa mapato katika kituo hicho,umeongezeka kwa asilimia zaidi ya 300 na kwamba kodi ya vibanda pia imeongezeka toka kati ya shilingi 25,000 hadi 50,000 kwa mwezi hadi 250,000 hadi 300,000 kwa mwezi.